# HALMASHAURI YA MJI MASASI

## MJI WETU-FAHARI YETU

Jarida la Mtandaoni | *Toleo na. 02* | *www. masasitc.go.tz* | Oktoba-Desemba 2023

## YALIYOMO



HABARI



MAKALA



MICHEZO


- Rasmi Zahanati za Matawale na Machombe Zaanza Kutoa Huduma, Mhe. Geoffrey Mwambe Azindua........................... *Uk. 02*
- Wajumbe wa Kamati Ya Bunge Wapongeza Ubora wa Kituo Cha Afya Mtandi.......................................................... *Uk. 03*
- "Tulipe Ushuru Wa Halmashauri" Mhe. Namtumba............. *Uk. 05*
- Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Unaenda Kwa Kasi, Baraza la Madiwani Lazungumza........................................ *Uk. 06*
- Viongozi kutoka Mamlaka ya Mji Mdogo Utete Mkoani Pwani Watembelea Halmashauri Ya Mji Masasi................................ *Uk. 08*
- Kiwango cha Ufaulu Elimu Msingi Chapaa, Dc Na Mbunge Watoa Pongezi.......................................................... *Uk. 09*
- "Wanafunzi Wote Waripoti Shuleni" Kanali Ahmed Abbas......... *Uk. 10*
- Wazazi Wahimizwa Kuchangia Upatikanaji wa Chakula Shuleni.. *Uk. 12*
- Watumishi Masasi Mji Kupimwa Utendaji Kazi Kidigitali......... *Uk. 13*
- Makala: Serikali ya Dkt Samia Imewasikia na Kuwafikia Wananchi wa Masasi Mji.............................................. *Uk. 14*


*Tembelea Tovuti yetu kupata Nakala yako/www.masasitc.go.tz*

# RASMI ZAHANATI ZA MATAWALE NA MACHOMBE ZAANZA KUTOA HUDUMA, MHE. GEOFFREY MWAMBE AZINDUA.




Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe, Geoffrey Mwambe amefungua rasmi zahanati mpya ya kijiji cha Matawale Kata ya Matawale, Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara ikiwa ni ndani ya siku sita tu toka alipofungua zahanati mpya ya Machombe.

Hatua hiyo ameeleza kuwa ni mafanikio makubwa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha wanan chi wa Masasi Mji wanapata huduma bora za afya kwenye maeneo yao.

Ameeleza hayo, Novemba 24, 2023 wakati wa ufunguzi rasmi wa zahanati ya Matawale iliyopokea fedha kiasi cha Tsh milioni 150 kutoka Serikali kuu zilizotolewa kwa awamu tatu.


Mhe. Mwambe amewataka watumishi katika zahati hiyo kuendelea kufanya kazi kwa kujitoa, ushirikiano, weledi na kuzingatia huduma bora sambamba na kuwaomba wanan chi kuwapa ushirikiano watumishi hao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanajiunga na bima ya afya yenye gharama ya Tsh 30000 tu kwa mwaka kwa familia.

Naye, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi, Mhe. Hashim Namtumba amesema kuwa huo ni mwendelezo wa kuhakikisha huduma bora za afya zinapatikana na kuimari ka na kwamba Halmashauri itakikisha inaendelea kuimarisha huduma za afya katika maeneo yote ya Mji Masasi.

Diwani wa kata ya Matawale, Mhe. Hamisi Mnela amesema ufunguzi wa kituo hicho ni alama kubwa kwa wananchi kwa kuwapunguzia umbali wa kutafuta huduma za afya huku akiwashukuru Wananchi, Rais Dkt Samia na Mbunge Mwambe kwa kuhakikisha zahanati hiyo inakamilika na kufunguliwa.

*Inaendelea... uk 3*

Kaimu Mkurugenzi wa Mji Masasi, Ndg. Andrea Kalinga amewapongeza wananchi wa kijiji cha Matawale kwa kujitoa kwa nguvu kuhakikisha ujenzi huo unafanikiwa kwaku wa mchango wao ni mkubwa ukiwa na thamani ya fedha kiasi cha zaidi ya Tsh milioni tatu.




Mkuu wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Dkt. Salum Gembe amesema zahana ti hiyo ni ya kisasa na bora na tayari watoa huduma za afya wameshaanza kutoa huduma katika zahanati hiyo.

Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi wilaya ya Masasi Ndg. Twahili Mayola akimwakilisha Mwenyekiti wa CCM wilaya, amesema wananchi wanashuhudia utekele zaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo.

Wananchi wa kata ya Matawale akiwemo Faraja Hamad na Subira Selemani wamesema ufunguzi wa zahanati unakwenda kuwa suluhisho la changamoto za afya na uzazi kwa mama na mtoto.

## WAJUMBE WA KAMATI YA BUNGE WAPONGEZA UBORA WA KITUO CHA AFYA MTANDI.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wamepongeza ubora wa miundo mbinu na vifaa tiba vya kutolea huduma za afya katika kituo cha afya Mtandi, Halmashauri ya Mji Masasi.

Aidha wamempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe. Geoffrey Mwambe kwa kupambana kwa nguvu kuhakikisha miradi mbalimbali ikiwemo kituo hicho inawafikia wananchi wote wa Masasi.

Pongezi hizo zimetolewa Novemba 13, 2023 mara baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Dennis Londo kutembelea na kukagua miundombinu.

*Inaendelea... uk 4*

Mjumbe wa Kamati hiyo, Mbunge Mwita Waitara amesema vifaa tiba katika kituo hicho vina ubora mkubwa na vya kisasa.

*" Mhe Mwenyekiti, Hapa wana mitambo ya kisasa kabisa, hapa tumepita Dental service inayotolewa hapa, kwangu kule sijaiona, hivyo nimepiga picha nikawaoneshe wenzangu kwamba kule Masasi, Mtwara Kuchelee..sasa hii kazi ya Mama Samia lazima tuiseme, wananchi wajue kwamba hapa kuna kituo cha kisasa chenye vifaa vya kisasa" Mjumbe wa Kamati, Mbunge Mwita Waitara.*

Naye, Mjumbe wa kamati hiyo, Profesa Palamagamba Kabudi amesema kituo hicho kinafaa kuwa hospitali.



*"Nami niungane na wenzangu wote kuipongeza kabisa Halmashauri ya Mji Masasi na Wilaya kwa kujenga kituo cha afya cha viwango vya hali ya juu, kwasisi wahenga hiki sio kituo cha afya, hii ni hospitali, kwakweli viwango vyake ni vya hospitali, kituo cha afya hiki baada ya miaka 10 au 15 kitakuwa hospitali. Rai yangu tujitahidi tujenge uzio"Mjumbe wa Kamati, Profesa Kabudi.*

Aidha kwa niaba ya Mwenyekiti, Mjumbe wa kamati hiyo, Mbunge Amandus Chinguile ametoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais na Mbunge wa Jimbo hilo.

*"Nilete salamu za Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini, Mhe. Geoffrey Mwambe, anafanya kazi nzuri sana, jamani hivi vitu havijileti huku kimiujiza, wako watu wanasema kwa niaba yenu, na huyo mtu ni mbunge wenu, anafanya kazi nzuri sana, anazungumza, anazunguka kwenye ofisi mbalimbali na anauzoefu mkubwa sana, hivi vimeletwa Masasi baada ya Mhe Mbunge kusema Masasi tunashida na kituo cha afya na nyingine nyingi" Mjumbe wa Kamati, Mbunge Chinguile.*

Aidha, Mjumbe wa Kamati hiyo, Mbunge Salome Makamba amesema ni vyema kuonge za upatikanaji wa umeme wa uhakika na maji katika kituo hicho.

*"Ujenzi wa Miundombinu katika kituo hiki upo vizuri sana, nashukuru sana mmefanya vizuri, ni sehemu ya kuigwa mfano, pamoja na hii tuboreshe tuwe na reserve ya maji pia umeme, hospitali hii ina vifaa vya kisasa naipongeza serikali lakini lingine ni muhimu kuwa na daktari wa dharula ambaye anakaa karibu na kituo cha afya " Mjumbe wa kamati, Mbunge Salome Makamba.*

Halikadhalika, Mjumbe wa kati hiyo, Mbunge Zuberi Kuchauka *Inaendelea... uk 5*

ameridhika na hali ya ujenzi wa kituo cha afya Mtandi.

*"Mimi niungane na wajumbe wenzangu, nimeridhika na hali ya ujenzi wa kituo cha afya hiki, tupo vizuri" Mjumbe wa kamati, Mbunge Zuberi Kuchauka.*

Katua nyingine, Mjumbe wa kamati hiyo Chinguile ameipongeza Serikali kupitia Ofisi ya Rais- Tamisemi kwa kazi kubwa ya kuwafikia wananchi wa maeneo yote nchini.

*"Na mimi niungane na waheshimiwa wabunge wenzangu kuwapongeza wenzetu Masasi lakini kipekee Mhe. Naibu Waziri Dkt. Festo Dugange, hii kazi kubwa na nzuri mmeifanya katika halmashauri hii, hongereni sana lakini pia ni jukumu letu kulinda miundombinu hii" Mjumbe wa Kamati Mbunge Amandus Chinguile.*

Ujenzi wa kituo cha afya Mtandi umegharimu kiasi cha Tsh milioni 500, fedha kutoka Serikali kuu.

## "TULIPE USHURU WA HALMASHAURI" MHE. NAMTUMBA.



*"Hili ni jukumu la kila mmoja wetu, kuanzia wananchi wenyewe, soko kwa ujumla, mtendaji wa mtaa,Mkurugenzi, Waheshimiwa madiwani wenzangu, Mimi Mwenyekiti wa Halmashauri, kila mmoja awajibike kwa nafasi yake, jambo hili sio la mtu mmoja" Mhe. Namtumba.*



**Mwenyekiti** wa Halmashauri ya Mji Masasi, Mhe. Hashim Namtumba Novemba 30,2023 ametembelea eneo la TK,ambapo amezungumza na abiria na madereva wa usafirishaji wa abiria ( daladala) sambamba na kukagua risiti za kielektroniki za halmashauri.

Mhe. Namtumba amewasisitiza madereva kuzingatia sheria, taratibu na kanuni za Serikali kwa kuhakikisha wanalipa tozo mbalimbali zinazotakiwa kwenye Halmashauri ili uteke lezaji wa miradi ya maendeleo uweze kufanikiwa kwa wakati na wananchi wapate hudu ma inayostahili.

Aidha ametembelea eneo ya stand ya Sokosela ambayo ni standi ya mabasi ya kuelekea vijijini ambapo amepokea na kusikiliza changamoto mbalimbali za stand hiyo kutoka kwa katibu wa sokosela na wananchi na kusema kwamba halmashauri itafanyia kazi changamoto zote muhimu za eneo hilo.

Inaendelea... uk 6

Sambamba na hilo, Mhe. Namtumba amefanya “Operationi ya Usafi wa Mji”kwa kutem belea, kukagua na kutathmini hali ya usafi wa mazingira katika maeneo yote ya soko na maeneo ya kukusanyia taka.

Mhe, Namtumba ametembelea na kutathmini hali ya usafi katika maeneo ya dampo la Soko la Tandale kata ya Jida, dampo la soko la Mkuti, dampo la Sokosela, eneo la uwa nja wa fisi, standi ambapo amezungumza na wazabuni, viongozi na wananchi.

Mhe. Namtumba amesema ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha hali ya Mji wa Masasi inakuwa safi kwa kuhakikisha Mzabuni anafanya kazi yake ipasavyo ikiwa ni sambamba na kuhakikisha anawalipa vibarua wake kwa wakati na kuzoa taka kupeleka mahali husika kwa wakati, lakini pia wananchi wanatakiwa kutoa fedha ya taka kwa wakati ili zoezi la uzoaji taka lifanyike kwa ufanisi.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO UNAENDA KWA KASI, BARAZA LA MADIWANI LAZUNGUMZA.



Baraza la Madiwani Halmashauri ya Mji Masasi likiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Hashim Namtumba limemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt, Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayowezesha ukuaji na ustawi wa wananchi wa Mji wa Masasi.

Aidha limemshukuru Mhe, Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe. Geoffrey Mwambe kwa kupambana na kuhakikisha miradi ya maendeleo inawafikia wananchi katika kata zote 14 za Halmashauri ya Mji Masasi.

Hayo yamebainishwa Novemba 8, 2023 katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Kwanza, 2023/2024 wa kupokea taarifa za kata uliofanyika katika Ukumbi wa Jengo la Utawala Halmashauri ya Mji Masasi.

Wajumbe wa kikao hicho waheshimiwa madiwani wa kata wameelezwa kuwa miradi mbalimbali ya zaidi ya shilingi bilioni moja katika kipindi cha Robo ya kwanza imeende lea kutekelezwa kwa kasi ikiwemo ujenzi wa shule ya sekondari kata ya Jida, Ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo shule ya msingi Mkomaindo, Ujenzi wa bwalo, madarasa na vyoo shule ya sekondari Mwengemtapika, ujenzi wa nyumba ya walimu shule ya

Inaendelea... uk 7

sekondari Temeke, ukamilishaji wa zahanati ya Napupa, ukamilishaji wa zahanati ya Matawale na Ujenzi wa Daraja Kata ya Marika.

Akizungumza Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe. Hashim Namtumba amesema utekelezaji wa miradi ya maendeleo unakuza Mji na kuimarisha maendeleo ya wananchi kiuchumi na kijamii.

"Taarifa ya kata ya Marika imewasilishwa na Diwani wa kata Mhe Asha Millanzi, Kiupekee kuhusu daraja linalounganisha kati ya Nanyumbu na Masasi naomba tumpong eze sana Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe Geoffrey Mwambe kwa namna ambav yo amepambana kuhakikisha daraja lile linakuwepo, kwanza ni daraja kubwa sana, linatufungulia mlango wa mapato na kwa umuhimu wake lile daraja kwa halmashauri yetu ni mlango wa uchumi kwasababu mazao yote"

Naye, Diwani Kata ya Mwengemtapika Mhe. Mussa Millanzi ameshukuru kwa kupata fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kata yake.

Ikumbukwe kuwa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Mji Masasi lina jumla ya madiwani 19, ambapo waheshimiwa Madiwani wa kata ni 14, viti maalumu 4 na Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini kama inavyobainisha orodha hapo chini.

| | |
|---|---|
| Mhe. Hashim Namtumba | Diwani Kata ya Jida (Mwenyekiti) |
| Mhe. Hamisi Nikwanya | Diwani Kata ya Mumbaka (M/Mwenyekiti) |
| Mhe. Ally Salvatory | Diwani Kata ya Mkomaindo |
| Mhe. Rashid Liundi | Diwani Kata ya Sululu |
| Mhe. Mbaraka Kodo | Diwani Kata ya Nyasa |
| Mhe. Hamisi Mnela | Diwani Kata ya Matawale |
| Mhe. Asha Millanzi | Diwani Kata ya Marika |
| Mhe. Frank Maranjila | Diwani Kata ya Temeke |
| Mhe. Valerian Mwajombe | Diwani Kata ya Mtandi |
| Mhe. Ismail Kalindima | Diwani Kata ya Migongo |
| Mhe. Bakari Namtubwi | Diwani Kata ya Mkuti |
| Mhe. Nicholaus Mpetula | Diwani Kata ya Chanikanguo |
| Mhe. Sospeter Nachunga | Diwani Kata ya Napupa |
| Mhe. Mussa Millanzi | Diwani Kata ya Mwengemtapika |
| Mhe. Maimuna Chiputa | Diwani Viti Maalum |
| Mhe. Ashura Nalino | Diwani Viti Maalum |
| Mhe. Shakila Lipetelo | Diwani Viti Maalum |
| Mhe. Benadetha Ndemanga | Diwani Viti Maalum |
| Mhe. Geoffrey Mwambe | Mbunge Jimbo la Masasi Mjini. |

## SIKU 75 TU ZATOSHA KUKAMILISHA MRADI WA NYUMBA YA WALIMU TEMEKE MASASI, MAZINGIRA YA UFUNDISHAJI YAZIDI KUBORESHWA.



**Nyumba** ya Walimu ya 2 in 1 iliyojengwa katika shule ya Sekondari Temeke Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara kwa gharama ya Tsh 94, 913,222 fedha kutoka Serikali kuu kupitia mradi wa SEQUIP imekamilika na tayari kuanza kutumika kutokana na kasi ya ujenzi kwa siku 75 tu.

Nyumba hiyo imekabidhiwa Desemba 4, 2023 na mkandarasi Shamsi hardware company limited kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mji, Afisa elimu sekondari, Bi. Elentruda Mtewele amesema nyumba hiyo imejengwa kwa ubora na kasi na kwamba inakwenda kuwasaidia walimu katika kukuza kiwango cha elimu.

Meneja wa mradi huo, Mhandisi wa Halmashauri ya Mji Masasi, Ndg. Ombeni Usiri amesema mradi huo ni wa miezi mitatu na ulianza kutekelezwa tarehe 20/9/2023 na ulitegemewa kukabidhiwa tarehe 18/12/2023 hivyo mradi umetekelezwa kwa muda wa siku 75 tu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Temeke akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi wa shule hiyo,amesema nyumba hiyo ni bora sana, wataitunza huku akimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za kuboresha mazingira ya ufundishaji, mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe, Geoffrey Mwambe kwa kuhakikisha miradi inafika kwa wananchi.

## VIONGOZI KUTOKA MAMLAKA YA MJI MDOGO UTETE MKOANI PWANI WATEMBELEA HALMASHAURI YA MJI MASASI



**Halmashauri** ya Mji Masasi imetembelewa na viongozi mbalimbali kutoka Mamlaka ya Mji Mdogo Utete kutoka Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani kwaajili ya kujifunza jinsi walivyovuka kutoka Mji Mdogo na kuwa Mji Kamili.

*Inaendelea... uk 9*

Mafunzo hayo yamefanyika Desemba 6,2023 katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji Masasi ambapo yamehusisha wenyeviti wa vitongoji Mamlaka ya Mji Mdogo, Diwani wa Kata ya chemchem, Kaimu mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi, Mkurugenzi wa Mji Masasi , Watalaamu kutoka Rufiji pamoja na watalaamu toka Halmashauri ya Mji Masasi.

Sambamba na mafunzo hayo wajumbe wamejifunza njia mbalimbali za ukusanyaji wa mapato, upangaji wa Mji, uongezaji na usimamizi thabiti wa vyanzo vya mapato pamoja na njia zinazotumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati.

Aidha walitembelea soko la Tandale kata ya Jida na Kituo cha Afya Mtandi kata ya Mtandi kwa ajili ya kujifunza na kujionea utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## KIWANGO CHA UFAULU ELIMU MSINGI CHAPAA, DC NA MBUNGE WATOA PONGEZI.

**Viongozi** mbalimbali wameipongeza Halmashauri ya Mji Masasi kwa kuo ngeza kiwango cha ufaulu kwa wana funzi wa elimu msingi kutoka asilim ia 68 za mwaka 2022 hadi asilimia 81 kwa mwaka 2023.

Pongezi hizo zimetolewa kwa nyakat i tofauti huku wakipongeza juhudi zi lizofanywa na Serikali katika kubore sha mazingira bora kwa walimu na m iundombinu ya ujifunzaji na ufundish aji.

Akizungumza katika maadhimisho y a miaka 62 ya Uhuru yaliyofanyika k atika Ukumbi wa shule ya Wasichana Masasi Desemba 9, 2023, Mkuu wa Wilaya ya Masasi Mhe.Lauter John Kanoni ameipongeza Halmashauri ya Mji Masasi kwa kuongeza kiwango cha ufaulu kwa elimu Msingi kutoka asilimia 68 mwaka 2022 hadi asilim ia 81 mwaka 2023.

“Tumepambana, tumezungushana, walimu tuka banana, mwaka huu Mungu si athumani, Halmashauri ya Mji Masasi wametoka kutoka asilimia 68 za ufaulu wa mwaka jana wamekwe nda asilimia 81, tuwapige makofi,Mkurugenzi nikupongeze na timu yako ni hatua kubwa sana hii, tuendelee kupambana ili tuwe halmashauri ya kwanza” DC Kanoni

Aidha, Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mh.Geoffrey Mwambe ametoa pongezi kwa Afisa Elimu Msingi pamoja na walimu kwa kufanikisha hilo huku akiwataka kuongeza jitihada za ufundishaji ili kuhakikisha ufaulu unaongezeka kwa asilimia 100.

Mhe. Mwambe alitoa pongezi hizo Desemba 7, 2023 katika kikao kilichofanyika ukumbi wa Shule ya wasichana Masasi kilicholenga kuha masisha juhudi za ufundishaji Mashuleni ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wote wenye madarasa ya Mitihani.

*“Ongezeni juhudi za ufundishaji*

*Inaendelea... uk 10*

*"na ufanisi katika kazi zenu ili tuongeze ufaulu kwa watoto wetu kwani juhudi zikionge zeka na matokeo yanakuwa mazuri katika Halmashauri yetu, lakini pia fanyeni kazi kwa bidii, jitoeni ili muonekane na Serikali kwani ukifanya kazi kwa kujitoa siku utaona Matunda ya kujituma utajikuta upo sehemu nyingine ambayo ni bora zaidi"Mhe Mwambe.*

Kwa upande wake, Afisa Elimu Msingi , Bi.Hamida Msemo ametoa shukrani za dhati kwa ushirikiano walioupata toka kwa Mh. Mbunge Jimbo la Masasi Mjini, Mhe. Mkuu wa Wilaya, Waheshimiwa Madiwani, Mkurugenzi wa Mji, Wakuu idara na vitengo Hal mashauri ya Mji, Wachungaji na Walimu wote na kuomba Ushirikiano huo uendelee ili idara ya Elimu Msingi ifanye kazi vizuri zaidi kwa 2024.

Kwa mwaka 2023 Halmashauri ya Mji Masasi ilikuwa na shule 44 zilizofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na kwa kuzingatia wastani wa alama za ufaulu kwa kila shule iliyofanya mtihani, miongoni mwa shule 10 za kwanza, ni shule ya Macdonald, Bezalel, Muzdalifa, Magumchila, Migongo, Sabasaba, Mkuti, Mkuti B, Maendeleo na Namatunu.

## "WANAFUNZI WOTE WARIPOTI SHULENI" KANALI AHMED ABBAS



**Mkuu** wa Mkoa wa Mtwara Mhe, Kanali Ahmed Abbas Ahmed amewataka wazazi kuhakikisha wanawapeleka wanafunzi wote waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule za sekondari bila kuwepo na kisingizio kwa kuwa serikali imejenga na kuboresha miundombinu ya kutosha shuleni.





Mhe, Kanali Ahmed amesema hayo wakati alipotembelea na kukagua ujenzi wa miund ombinu ya elimu katika Halmashauri ya Mji Masasi kwaajili ya kuhakikisha kuwa inaka milika na kupokea wanafunzi kuanzia Januari 8, 2024.

Mhe. Kanali Ahmed ametembelea miradi hiyo Desemba 22, 2023 ambapo amekagua ujenzi wa shule ya sekondari Jida inayojengwa kupitia mradi wa SEQUIP na Ujenzi wa Shule ya Msingi Darajani iliyojengwa kupitia mradi wa Boost.

Amesema Ujenzi wa miundombinu hiyo unaofanywa na Serikali ya awamu ya sita inay oongozwa na Mhe,Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ni katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza na elimu ya msingi *Inaendelea... uk 11*

wanapata nafasi ya kusoma katika mazingira bora na kisasa.
Aidha amewapongeza wananchi, Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini, Diwani na viongozi wa serikali kwa kuhakikisha wanasimamia vyema utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo.

Wakizungumza katika ziara hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi ambaye pia ni Diwani kata ya Jida,Mhe Hashim Namtumba na Diwani kata ya Mkomaindo Mhe, Ally Salvatory wamesema ujenzi wa miundombinu hiyo katika kata zao unakwenda kuwa suluhisho la kudumu la upatikanaji wa elimu bora kwa wanafunzi wa maeneno ya karibu na kata za jirani.

## DC KANONI AKABIDHI VIBAO VYA KUPIMA UREFU/KIMO KWA WATOTO.

**Mkuu** wa wilaya ya Masasi Mhe. Lauter John Kanoni amemkabidhi Mkurugenzi wa Mji Masasi Ndg. Reuben Sixbert Jichabu vibao nane vya kupima urefu/kimo kwa watoto chini ya miaka 5 ambavyo vitasaidia kutambua hali ya udumavu kwa watoto katika vituo vya kutolea huduma za afya Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara.




Mhe. Kanoni alikabidhi vibao hivyo katika kikao cha tathmini ya Lishe Robo ya kwanza 2023/ 2024 kilichofanyika katika Ukumbi wa Jengo la Utawala halmashauri ya Mji Masasi.

Kikao hicho kilihudhuriwa na kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya, Watendaji wa kata 14 za halmashauri ya Mji Masasi, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wawakilishi kutoka Taasisi za dini, Maafisa Lishe na watoa huduma wa vituo vya kutolea huduma za afya.

## KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA YATEMBELEA NA KUKAGUA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO.



**Kamati** ya Fedha na Utawala Halmashauri ya Mji Masasi Oktoba 27, 2023 imefanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

*Inaendelea... uk 12*

Kamati hiyo imetembelea na kukagua miradi inayotekelezwa kwa fedha kutoka Serikali kuu na fedha kupitia mradi wa SEQUIP ambao ni mradi wa uboreshaji wa elimu ya sekondari wenye lengo la kuhakikisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanaboreshwa katika shule za sekondari.

Kamati imetembelea,Ujenzi wa nyumba 1 kwa 2 ya walimu shule ya Sekondari ya kutwa Temeke – Masasi unaotekelezwa kwa fedha za Sequip kwa gharama ya Tsh. 95,000,000.

Kamati pia imekagua Ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Jida unaotekelezwa kwa fedha za Sequip kwa gharama ya Tsh. 560,552,872.

Aidha wametembelea na kukagua, Ukamilisha wa Ujenzi wa Zahanati ya Napupa unaotekelezwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu kwa gharama ya Tsh. 50,000,000.

Ujenzi wa Vyumba 9 vya madarasa na Matundu 16 ya vyoo vya Shule ya Msingi Mkomaindo unaotekelezwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu kiasi cha Tsh. 208,000,000.

Ukamilishaji wa Ujenzi wa Zahanati ya Matawale unaotekelezwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu kwa gharama ya Tsh.150,000,000.

Pia imetembelea na kukagua Ujenzi wa Bwalo, Madarasa na Vyoo shule ya Sekondari Mwengemtapika unaotekelezwa na fedha kutoka Serikali Kuu kwa gharama ya Tsh 320,000,000.

Kamati hiyo inayoongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi Mhe. Hashim Namtumba na wajumbe imeridhishwa na Utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaosimamiwa na watalaamu chini ya Mkurugenzi wa Mji Masasi Ndg. Reuben Sixbert Jichabu sambamba na kumpongeza Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe, Geoffrey Mwambe kwa kuhakikisha miradi inafika kwa wananchi wote wa Masasi Mji na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Dkt, Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoka fedha za utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kwa wananchi.

## WAZAZI WAHIMIZWA KUCHANGIA UPATIKANAJI WA CHAKULA SHULENI



Diwani kata ya Napupa halmashauri ya Mji Masasi Mhe. Sospeter Nachunga amewaomba wazazi na walezi wa shule ya msingi Kambarage na kata ya Inaendelea... uk 13

Napupa kiujumla kuchangia upatikanaji wa chakula shuleni ili kukuza maendeleo ya elimu.

Ameeleza hayo Oktoba 18,2023 katika kikao cha wazazi kilichofanyika Shule ya MsingiKambarage na kuhudhuriwa na viongozi wa Chama cha mapinduzi, Walimu, Afisa elimu ya awali na msingi, wazazi, wanafunzi na wadau mbalimbali.

Mhe. Nachunga ameeleza kuwa chakula kikitolewa Mashuleni kitaongeza ufaulu, watoto watapenda shule na Maendeleo ya elimu yataongezeka zaidi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Afisa Tarafa halmashauri ya Mji ma sasi, Ndg. Fikiri Lukanga amewaomba wazazi kuona umuhimu wa kuchangia chakula Shuleni kwa ajili ya utekelezaji wa lishe bora ili kuong eza ufaulu kwa wanafunzi .

Kwa upande wake, Afisa Elimu ya Awali na M singi Halmashauri ya Mji Masasi Bi. Hamida Msemo amesema kikao hicho kina lengo mahu susi la kuhamasisha wazazi kuchangia upatikan aji wa chakula Shuleni.

*"Kila mzazi anatakiwa kuchangia chakula shuleni ili watoto wetu wapate chakulashuleni" Mzazi*

Naye, Mzazi na Mkazi wa Kata ya Napupa, Ndugu. Juma Mtinga amesema kama wazazi wana jukumu la kuhakikisha kila mzazi anachangia chakula ili wanafunzi wasome shuleni.

## WATUMISHI MASASI MJI KUPIMWA UTENDAJI KAZI KIDIGITALI



**Mkuu** wa Idara ya Utawala na utumishi Halmashauri ya Mji Masasi Bi. Renalda Mbowe amewataka watumishi kujisajili kwenye mfumo wa kidigitali wa kupima utendaji kazi wa watumishi wa umma (PEPMIS) ili kuboresha utendaji wa kazi.

Amesema ili mtumishi aweze kujisajili na kutumia mfumo huo ni lazima ajisajili kw anza kwenye mfumo wa "ess.utumishi.go.tz" ambao utamuwezesha kutumia mfumo wa PEPMIS.



Amesema hayo Novemba 28, 2023 wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya mfumo huo yaliyofanyika katika Ukumbi wa Jengo la Utawala.

Amesema mfumo huo umekuja kuboresha utendaji kazi kwa watumishi wa umma kwa ngazi zote za utendaji na kila mtumishi atapimwa utend aji wake wa kazi kupitia mfumo huo.

Aidha mafunzo hayo yametolewa Novemba 29, 2023 ambapo kiujumla yamehudhuriwa na Wakuu wa Idara na Vitendo, Watumishi wote wa HQ, Watumishi wa Afya, wakuu wa shule, Walimu, Maafisa elimu kata na watumishiwa idara zote za Halmashauri ya Mji Masasi wamepatiwa mafunzo ayo.

**MAKALA**

# SERIKALI YA DKT SAMIA IMEWASIKIA NA KUWAFIKIA WANANCHI WA MASASI MJI

**Mkurugenzi** wa Halmashauri ya Mji Masasi, Ndg. Reuben Sixbert Jichabu amesema Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imewasikia na kuwafikia wananchi wa Mji Masasi kwa kutoa jumla ya shilingi 13,847,872,949 kwa ajili ya utekekezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo miradi ya Elimu, Afya, Kilimo, Mifugo, Utalii, Viwanda na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Amesema viongozi wa Halmashauri kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe, Geoffrey Mwambe na Wahe.Madiwani wataendelea kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo unawanufaisha wananchi wa Masasi.

Amesema hayo wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa waandishi wa habari na ofisi ya Idara ya Habari maelezo katika mkutano uliofanyika Desemba 19, 2023 katika ukumbi wa BOT Mtwara. Kwa upande wa elimu, amesema jumla ya fedha Sh.3,679,203,376 zimepokelewa na kutekeleza miradi mbalimbali ya elimu.Aidha amesema Halmashauri imepokea jumla ya fedha Sh.682,300,000 kutoka Mradi wa boost kwa ajili ya Ujenzi wa Miundombinu ya shule za Msingi.

*Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuwasikia na kuwafikia wananchi wa Masasi Mji kwa kutuletea fedha nyingi za utekelezaji wa miradi ya Maendeleo.*

*Sisi kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo la Masasi Mji Mhe. Geoffrey Mwambe, Mkuu wa Mkoa Mhe, Kanali Ahmed Abbas, Mkuu wa Wilaya Mhe, Lauter Kanoni, Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe. Hashim Namtumba na Waheshimiwa Madiwani na viongozi wote tutaendelea kusimamia na kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo unawafikia wananchi wote wa Halmashauri ya Masasi Mji.*


Mkurugenzi wa Mji Masasi, Ndg. Reuben Sixbert Jichabu akizungumza na waandishi wa Habari Desemba 19, 2023 Mkoani Mtwara.

Amesema jumla ya fedha Sh.1,254,300,000 zimepokelewa kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ambapo amesema Kati ya hizo Sh.366,400,000 zimetumika kujenga vyumba 17 vya madarasa na matundu 24 ya vyoo katika shule 6 , ujenzi wa miundo mbinu shule kongwe ya Masasi wasichana Sh.387,900,000, na ujenzi wa madarasa 5 na bwalo ya kidato cha tano katika shule ya sek ondari Mtapika Sh.320,000,000, pamoja na Sh.180,000,000 za ukamilishaji wa maabara katika sekondari ya Masasi Kutwa, Anna abdalah na Chanikanguo.

Sambamba na hilo amesema Sekta ya afya imeendelea kutekelezwa kwa vitendo ambapo jumla ya fedha Sh 2,615,000,029 zimepokelewa na kutekeleza miradi mbalimbali katika vituo vya kutolea huduma ya afya.

Amesema Jumla ya fedha Sh.300,000,000 zimepokelewa kwa ajili ya kujenga Jengo la kutolea huduma za dharura(emergency) katika Hospitali ya Mkomaindo. Jumla ya fedha Sh. 500,000,000 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha Mtandi

Aidha Jumla ya fedha Sh.115,000,029 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi(3 kwa1 ) zahanati ya Namatunu Sh. 95,000,000 pamoja na ukarabati wa wodi ya wagonjwa wanaotengwa hospitali ya Mkomaindo Sh.25,000,029.04. Ameongeza kuwa Sh.900,000,000 ni kwa ajili ya Ukarabati wa Hospitali ya Mkomaindo, Sh. 200,000,000 ni za ujenzi wa zahanati za matawale na Napupa pamoja na Sh.600,000,000 za ununuzi wa vifa tiba katika vituo vya afya 2 na zahanati 3

Halmashauri ya Mji Masasi katika kipindi cha uongozi cha awamu ya sita (6) imefanikisha kuongeza idadi ya vikundi vilivyosajiliwa kutoka vikundi 75 mwaka 2020/21 hadi 118 kufikia Dec 2023. Vikiwemo vikundi vya wanawake 68, vijana 44 na wenye ulemavu vikundi 6.

Kiasi kilichokopeshwa katika kipindi cha awamu ya sita (6) ni Sh. 661,350,326 ambapo wanawake wamekopeshwa Sh.398,050,326.00 vijana wamekopeshwa Sh.237,300,000 na wenye ulemavu wamekopeshwa Sh.26,000,000.00

Katika kipindi cha awamu ya 6, Halmashauri imepokea fedha za kutekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini pamoja na utoaji wa ajira kwa walengwa TASAF Sh.3,797,994,709
.

# MICHEZO

## MAADHIMISHO YA MIAKA 62 YA UHURU

**Maadhimisho** ya Miaka 62 ya Uhuru katika Wilaya ya Masasi yamefanyika yakihusisha Shughuli mbalimbali ikiwemo michezo kama Mpira wa miguu, Mashindano ya Insha kwa shule za msingi na sekondari sambamba na kupanda miti katika maeneo mbalimbali.

Katika mchezo wa mpira wa miguu uliochezwa katika Uwanja wa Boma Desemba 9, 2023 Wahuva Sports Club waliibuka kidedea kwa changamoto ya mikwaju ya penati 5-3 dhidi ya Maendeleo Fdc.


Mkuu wa Wilaya ya Masasi Mhe, Kanoni akigawa zawadi kwa mshindi wa kwanza wa mpira


Mkuu wa Wilaya ya Masasi Mhe, Kanoni Desemba 9, 2023 akigawa zawadi kwa mshindi wa kwanza Insha sekondari


Mkuu wa Wilaya ya Masasi Mhe, Kanoni Desemba 9, 2023 akigawa zawadi kwa mshindi wa Insha shule ya msingi


Katibu Tawala Wilaya ya Masasi Bi. Fatma Kubenea akiongoza zoezi la kupanda miti s/m Nangose ikiwa ni shamrashamra za uhuru


Afisa elimu Msingi H/Mji Masasi Bi. Hamida Msemo akipanda miti katika zoezi la kupanda miti s/m Nangose ikiwa ni shamrashamra za uhuru


Afisa Tarafa Mji Masasi Fikiri Lukanga akipanda miti katika zoezi la kupanda miti s/m Nangose ikiwa ni shamrashamra za uhuru







Watumishi wa Halmashauri ya Mji Masasi wakifanya usafi katika hospitali ya Mkomaindo ikiwa ni shamrashamra za maadhimisho ya miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara Desemba 9, 2023.

Zawadi kwa washindi mbalimbali ikiwemo mbuzi kwa mshindi wa kwanza wa mpira wa miguu zilikabidhiwa na Mkuu wa Wilaya ya Masasi Mhe. Lauter John Kanoni katika Ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Masasi Desemba 9, 2023.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Mhe, Ummy Nderiananga Novemba 22, 2023 apokea na kugawa vifaa saidizi kwa ajili ya watu wenye ulemavu Mkoa wa Mtwara.



Mamia ya wananchi waliohudhuria kwenye uzinduzi wa zahanati ya Machombe uliofanywa na Mbunge wa Masasi Mjini Mhe, Geoffrey Mwambe Novemba 18, 2023



Waheshimiwa Madiwani Halmashauri ya Mji Masasi wakiwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Novemba 8, 2023.



Makamu Mwenyekiti H/Mji Masasi Mhe Hamisi Nikwanya kwa kushirikiana na Idara ya Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii wakimkabidhi baskeli ya kutembelea Bw. Jafari Abdalllah Mrope mkazi wa kijiji cha Namikunda .



Kaimu Mkurugenzi Mji Masasi, Ndg. Andrea Kalinga Novemba 30, 2023 akizindua kampeni ya utoaji chanjo kwa watoto waliokosa na waliohasi chanjo



Mwenyekiti H/Mji Masasi, Mhe. Hashim Namtumba Novemba 09, 2023 akizindua jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi ngazi ya Halmashauri.



Maandamano ya Kilele cha Kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia Novemba 25-Desemba 10, 2023.

## OFA KWA WATUMISHI WA UMMA NA WANANCHI WOTE

TAREHE: 28/12/2023

### TANGAZO LA UUZAJI WA VIWANJA

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI MASASI ANAPENDA KUWATANGAZIA WATUMISHI WOTE WA MAKAMPUNI, TAASISI ZA SERIKALI NA BINAFSI KUWA HALMASHAURI YA MJI MASASI INAUZA VIWANJA VILIVYOPIMWA KWA MATUMIZI MBALIMBALI. VIWANJA HIVYO VINAPATIKANA KATIKA ENEO LA MAILISITA KATA YA CHANIKANGUO KATIKA MRADI WA MAILISITA (MAILISITA PROJECT).

MCHANGANUO WA MATUMIZI YA ARDHI NA BEI VIMEAINISHWA KWENYE JEDWARI HAPO CHINI.

| S/N | MATUMZI | BEI KWA MITA MOJA YA MRABA |
|---|---|---|
| 1. | MAKAZI | 2,500 |
| 2. | MAKAZI NA BIASHARA | 2,700 |
| 3. | HUDUMA ZA JAMII | 3,000 |

FOMU ZA MAOMBI ZITAANZA KUTOLEWA OFISI YA ARDHI, HALMASHAURI YA MJI MASASI KUANZIA TAREHE 02/01/2024 HADI TAREHE 06/01/2024, KWA GHARAMA YA SHILINGI ELFU TANO (TSH 5,000/=) AMBAYO **HAITARUDISHWA.**

AIDHA, KWA ATAKAYECHUKUA FOMU ATATAKIWA KULIPA MALIPO YA AWALI KWA **15%** YA BEI NA BAADA YA MALIPO YA AWALI MTEJA ATAENDELEA KUFANYA MALIPO KUPITIA MSHAHARA WAKE KWA KILA MWEZI MPAKA PALE ATAKAPO MALIZA MALIPO NA KUKABIDHIWA KIWANJA.

NYOTE MNAKARIBISHWA.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI MASASI.

REUBEN S. JICHABU
MKURUGENZI WA MJI
MASASI

*Jarida la Mtandaoni limeandaliwa na,*
*Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*
*Halmashauri ya Mji Masasi*